

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI

05 MEI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI – TAREHE 05 MEI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAJI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**248. MHESHIMIWA CORNEL LUCAS MAGEMBE
(CHATO KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa Shule za Msingi Nyamirembe, Nyabugere, Katende na Magiri ambazo zimechakaa sana.

**249. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY
KISWAGA (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara za Mitaa Miji ya Kisesa na Bujora kwa kuwa ni Miji ya Kibiashara.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**250. MHESHIMIWA SELINA HENRY KINGALAME (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaajiri Wahitimu Wahadhiri wa Vitendo wanaojitolea sehemu za Ofisi na Vyuo hasa waliojitolea kwa zaidi ya mwaka.

WIZARA YA KILIMO:

251. MHESHIMIWA JAPHAEL MASANJA LUFUNGIJA (ULYANKULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Maghala ya kuhifadhia Mazao Kata ya Uyowa katika Kitovu cha biashara Mwamnange ambapo tayari eneo lipo.

WIZARA YA MAJI:

252. MHESHIMIWA DKT. SELEMANI SAIDI JAFO (KISARAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa maji kutoka Kisarawe Mjini kwenda Kata za Kazimzumbwi, Masaki, Msimbu, Kibuta hadi Marumbo utanza kujengwa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

V. HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. WILLIAM SAMOEI RUTO, RAIS WA JAMHURI YA KENYA:

VI. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
05 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**

